**Mapendekezo Ya Tume Ya Ugavi Wa Mapato Kuhusu Mgao Wa Mapato Kati Ya Serikali Ya Kitaifa Na Serikali Za Ugatuzi**

**2nd November 2021**: Tume ya ugavi wa mapato (CRA) leo imetoa mapendekezo ya ugavi sawa wa mapato kati ya serikali ya kitaifa na serikali za ugatuzi kwa kipindi cha mwaka wa kifedha 2022/2023.

Tume inapendekeza kuwa: kulengana na makadirio ya mapato ya kima cha shilingi bilioni 2,142 ya mwaka wa kifedha wa 2022/23, serikali ya kitaifa ipate mgao wa shilingi bilioni 1,765.2 na serikali za ugatuzi zipate shilingi bilioni 370 na nyongeza ya shilingi bilioni 6.8 kwa mfuko wa usawazishi. Mgao wa serikali za ugatuzi ni sawa na asilimia 27.3 ya taarifa za fedha za punde Zaidi zilizokaguliwa za mwaka wa kifedha wa 2016/17 ambazo ni kima cha shilingi bilioni 1,357.7

Tume inapendekeza pia kua makadirio ya ongezeko la mapato la kima cha shilingi bilioni 366.4 zaidi ya makadirio ya shilingi bilioni 1,775.6 ya mwaka wa kifedha a 2021/22 yatakapoafikiwa basi fedha hizo zitumike kupunguza nakisi ya kifedha kwa mujibu wa maslahi ya kitaifa.

Mgao wa mapato wa mwaka wa 2022/23 unatarajiwa kuongezeka kwa kima cha shilingi bilioni 366.4 kutoka makadirio ya shilingi bilioni 1,775.6 ya mwaka wa 2021/22 hadi bilioni 2,142. Tume imezingatia pia kwamba kwa kuwa kiwango cha mapato kimebaki chini ya makadirio kwa miaka tisa mtawalia ya ugatuzi,serikali ya kitaifa imekuwa ikigaramia nakisi ya mapato hayo hiiikitokana na sheria ya ugavi wa mapato ambayo hulinda mgao wa kaunti usibadilishwe. Kugaramia nakisi ya mapato huathiri nakisi ya kifedha ya serikali ya kitaifa na hatimaye ongezeko la deni la umma.